# SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

# OFISI YA RAIS FEDHA NA MIPANGO

# TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI YA SERIKALI KWA KIPINDI CHA JULAI – JUNI 2022/2023

**Ogasti, 2023**

**YALIYOMO:**


MAPITIO YA BAJETI KWA KIPINDI JULAI – JUNI 2022/2023 ---------------------------------------------- 1

UTANGULIZI ------------------------------------------------------------------------------------------------------------ 1

1. HALI YA UCHUMI ------------------------------------------------------------------------------------------------- 1

1.1 Mwenendo wa hali ya Uchumi-------------------------------------------------------------------------------- 1

1.2 Sekta ya Utalii---------------------------------------------------------------------------------------------------- 1

1.3 Sekta ya Nje ------------------------------------------------------------------------------------------------------ 2

1.4 Hali ya Mfumko wa Bei ---------------------------------------------------------------------------------------- 3

1.5 Miradi ya Uwekezaji na nafasi za Ajira--------------------------------------------------------------------- 4

1.6 Hali ya Upatikanaji wa Ajira Nchini ------------------------------------------------------------------------ 4

1.7 Viwango vya ubadilishaji wa Fedha ------------------------------------------------------------------------ 5

2. UTEKELEZAJI MPANGO WA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA ---------------------------------- 6

JULAI – JUNI 2022/2023---------------------------------------------------------------------------------------------- 6

3. UTEKELEZAJI WA BAJETI JULAI - JUNI 2022/2023------------------------------------------------------ 7

3.1 MAPATO ---------------------------------------------------------------------------------------------------------- 7

3.1.1 Mapato ya Ndani ---------------------------------------------------------------------------------------------- 7

3.1.2 Mapato Mengineyo -------------------------------------------------------------------------------------------- 7

3.1.3 Utekelezaji Halisi ---------------------------------------------------------------------------------------------- 8

3.2 MATUMIZI --------------------------------------------------------------------------------------------------------10

3.3 DENI LA TAIFA---------------------------------------------------------------------------------------------------12

3.4 HITIMISHO --------------------------------------------------------------------------------------------------------13

# MAPITIO YA BAJETI KWA KIPINDI JULAI – JUNI 2022/2023

## UTANGULIZI

Utekelelezaji wa bajeti kwa kipindi cha Julai-Juni mwaka wa fedha 2022/2023. yatajumuisha taarifa za mwenendo wa uchumi wa Zanzibar kwa kipindi kilichoishia Julai 2023, Utekelezaji wa Mpango wa Taifa na hatimae Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali , ikihusisha mapato na matumizi katika kipindi cha Julai – Juni mwaka wa fedha, 2022/2023.

## 1. HALI YA UCHUMI

### *1.1Mwenendo wa hali ya Uchumi*

Kwa mwaka 2022, kasi ya ukuaji uchumi imeongezeka na kufikia thamani ya TZS 3,499 bilioni mwaka 2022 kutoka thamani ya TZS 3,275 bilioni mwaka 2021.Aidha, Pato la Taifa kwa bei ya soko (GDP at current price) limeongezeka na kufikia thamani ya TZS 5,400 bilioni mwaka 2022 kutoka thamani ya TZS 4,633 bilioni mwaka 2021. Kwa mujibu wa takwimu hizo uchumi wa Zanzibar unaendelea kuimarika na umefikia ukuaji wa wastani wa asilimia 6.8 mwaka 2022 ukilinganisha na wastani wa asilimia 5.1 mwaka 2021.

### *1.2 Sekta ya Utalii*

Jumla ya watalii walioingia nchini katika kipindi cha Julai-Juni mwaka 2022/23 wamefikia watalii 627,339. kutoka watalii 408,590. katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22 sawa na ongezeko la asilimia 53. Ongezeko hili limesababishwa na

- ❖ Jitihada kubwa zinazochukuliwa na Serikali na Wadau wa utalii ambao kwa pamoja wanaufanya utalii wa Zanzibar kuimarika;

- Kuwepo kwa hali ya amani na utulivu wa kisiasa kumepelekea kuwavutia wageni wengi kuitembelea Zanzibar;

- Kuongezeka kwa Mawakala wa usafirishaji watalii (Tui- Tourism Union International na African Tours &Travel Companies.),pamoja kuitangaza Zanzibar kiutalii kwa kutumia njia mbali mbali ikiwemo kushiki katika maonyesho ya Utalii nje ya nchi na makongamano ya kibiashara katika mataifa mbali mbali ;

- Mabalozi wa Tanzania nje ya nchi kuendelea kufanya kazi nzuri ya kuutangaza utalii wetu na kusimamia sera ya Serkali katika kukuza na kuendeleza utalii nchini;

- Kuimarika kwa huduma za usafiri zilizozorota kipindi cha Uviko 19 ambapo kwa kiasi kikubwa kumepelekea mashirika ya ndege kurejesha huduma zao na kuongezeka kwa mashirika mapya ya ndege yanayofanya safari za moja kwa moja hadi Zanzibar yakiwemo Polish Airline, Azur Airline, Inter Airline, Eurowings Discover Airline, Airfrance na Edelweiss Airline

- Kuimarika kwa huduma za viwanja vya ndege hasa “Terminal 3” ya Uwanja wa ndege wa kimataifa wa Abeid Amani Karume pamoja na kuwepo kwa Kampuni ya Ground handling ambayo inatoa huduma stahiki.

- Kuendelea kufunguliwa kwa miradi mikubwa ya kitalii yakiwemo mahoteli ya nyota tano ambayo yanauwezo mkubwa wa kupokea wageni kama vile Hotel Riu Jambo na Emerald Zanzibar Resort & Spa; na

- Kuja kwa meli kubwa za kitalii nchini Crew ship na Watu maarufu Zanzibar wakiwemo wachezaji wa mpira wa miguu wa kimataifa.

## *1.3Sekta ya Nje*

### *1.3.1 Uingizaji wa Bidhaaa*

Katika kipindi cha Julai- Juni 2022/23, nakisi ya biashara imeongezeka hadi kufikia thamani ya TZS 1,206.9 Bilioni ikilinganishwa na thamani ya TZS 899.3

bilioni katika kipindi kama hicho mwaka 2021/22, hii ni kutokana na kuongezeka kwa uagizaji mkubwa wa bidhaa zinazoingia nchini.

Uagizaji wa bidhaa nchini kwa kipindi cha Julai- Juni 2022/23, umeongezeka hadi kufika thamani ya TZS 1,356.2 Bilioni ikilinganishwa na thamani ya TZS 1,105.4 Bilioni kwa kipindi kama hicho mwaka 2021/22, hali hii ni kutokana na kuongezeka kwa uagizaji mkubwa wa bidhaa hasaza nishati ya mafuta, bidhaa za chakula na bidhaa nyenginezo zikiwemo vifaa vya ujenzi.

#### *1.3.2 Usafirishaji wa Bidhaa*

Katika kipindi cha Julai- Juni 2022/23, Usafirshaji wa bidhaa kweda nje ya nchi umefikia thamani ya TZS 149.2 Bilioni ikilinganishwa na thamani ya TZS 206.0 Bilioni katika kipindi hicho mwaka 2021/22, kupungua kwa thamani ya usafirishaji wa bidhaa mwaka 2022/23 ni kutokana na kupungua kwa usafirishaji wa zao la karafuu kufikia tani 3,958.5 zenye thamani ya USD 32.2 Milioni mwaka 2022/23 kutoka tani 8,321.6 zenye thamani ya USD 60.5 Milioni mwaka 2021/22.

### *1.4 Hali ya Mfumko wa Bei*

Kasi ya mfumko wa bei imeongezeka kufikia wastani wa asilimia 6.9 katika kipindi cha Julai-Juni mwaka 2022/23 ukilinganisha na wastani wa asilimia 2.9 kipindi kama hicho mwaka 2022. Hali hii imetokana na kuongezeka kwa bei za bidhaa za chakula na zisizo za chakula. Katika kipindi cha Julai-Juni 2022/23 mfumko wa bei kwa bidhaa za chakula ulifikia wastani wa asilimia 10.02 kutoka watani wa asilimia 1.6 mwaka 2021/22 na bidhaa zisizo za chakula kufikia wastani wa asilimia 4.8 ukilinganisha na wastani wa asilimia 3.9 mwaka 2021/22.

Hata hivyo, Ongezeko hilo limesababishwa na kupanda kwa bei za vyakula na kuongezeka kwa gharama za usafirishaji na kupanda kwa Dola ya Kimarekani

dhidi ya shilingi ya Tanzania. Aidha Benki kuu iliweka mikakati madhubuti ya sera ya fedha kwa kuweka kiwango cha fedha za kigeni kinachohitajika katika uchumi ili kupunguza shinikizo la mahitaji ya ndani kwa fedha za kigeni dhidi ya ununuaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi . Vilevile, kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa za chakula kumetokana na kupungua kwa uzalishaji wa bidhaa za ndani za chakula.

### *1.5 Miradi ya Uwekezaji na nafasi za Ajira*

Jumla ya miradi iliyoekezwa nchini kwa mwaka 2022 imefikia miradi 93 yenye thamani ya TZS 4.5 trilioni kutoka miradi 97 yenye thamani ya TZS 2.6 trilioni katika kipindi kama hicho mwaka 2021 sawa na ongezeko la thamani ya wastani wa asilimia 73.0. Miradi hii imesaidia kutoa ajira mpya 3,970 mwaka 2022 ambapo miradi ya hoteli na migahawa imechangia wastani wa asilimia 31.2, ikifuatiwa na miradi ya uwekezaji wa nyumba za biashara (real estate) kwa wastani wa asilimia 22.7, miradi ya usafirishaji na uhifadhi imechangia wastani wa asilimia 10.0, miradi ya shughuli za ujenzi imechangia asilimia 9.6, miradi ya kilimo na misitu imechangia asilimia 9.1, miradi ya uzalishaji viwandani imechangia asilimia 5.1, na miradi mengineyo (miradi ya uvuvi; habari na mawasiliano; elimu; afya; biashara za jumla na rejareja, umeme na gesi) imechangia wastani wa asilimia 11.9 za ajira nchini. Aidha, Serikali inaendelea na jitihada za makusudi kuitangaza Zanzibar kwa mataifa mbali mbali ili kuimarisha uwekezaji sambamba na kuendelea kuwawekea mazingira mazuri wawekezaji wote wa ndani na nje ya nchi ili kuwekeza miradi yao kwa maendeleao endelevu ya Zanzibar.

### *1.6 Hali ya Upatikanaji wa Ajira Nchini*

Kwa mwaka 2022, jumla ya ajira mpya zilizopatikana ni 68,632 kutoka ajira 66,656 mwaka 2021.

- Ajira kutoka Serikalini zimefikia 37,189 (wanaume ni 15,541 na wanawake ni 21,648).
- Ajira kutoka Mashirika ya Serikali zimefikia 6,887 (wanaume ni 4,522 na wanawake ni 2,365), na
- Ajira binafsi zimefikia 24,556 (wanaume ni 15,947 na wanawake ni 8,609).

Kuongezeka kwa idadi ya ajira mpya mwaka 2022 kumetokana na kuongezeka kwa uhitaji mkubwa wa wafanyakazi katika sekta mbali mbali nchini.

### *1.7 Viwango vya ubadilishaji wa Fedha*

Katika kipindi cha Julai-Juni mwaka 2022/23 fedha ya Tanzania ilibadilishwa kwa wastani wa TZS 2,310.22 kwa Dola moja ya kimarekani (USD) ikilinganishwa na wastani wa TZS 2,298.13 katika kipindi kama hicho cha mwaka 2021/22. Shilingi ya Tanzania imepungua thamani kwa asilimia 0.5 hii ni kutokana na mtikisiko wa kiuchumi wa dunia ya sera ya "Dolarization" miamala yote ya fedha kufanyika kwa Dola za Kimarekani. Kwa upande wa Benki kuu ya Tanzania iliweka mikakati madhubuti ya Sera ya fedha ili kupunguza ukwasi na kuweka kiwango cha fedha kinachohitajika katika uchumi na kulinda shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola. Aidha, Dola za Kimarekani dhidi ya Shilingi ya Tanzania bado imeendelea kua himilivu kutokana na nguvu za sarafu nyengine duniani.

kwa upande wa sarafu nyengine, Pound moja ya Uingereza ilibadilishwa kwa wastani wa TZS 2,781.22 mwaka 2022/23 ikilinganishwa na wastani wa TZS 3,061.06 katika kipindi kama hicho cha mwaka 2021/22. Euro moja ilibadilishwa kwa wastani wa TZS 2,418.88 mwaka 2022/23 ikilinganishwa na wastani wa TZS 2,593.27 katika kipindi kama hicho cha mwaka 2021/22. Rupia moja ya India ilibadilishwa kwa wastani wa TZS 28.31 mwaka 2022/23 ikilinganishwa na wastani wa TZS 30.50 katika kipindi kama hicho cha mwaka 2021/22. Yuan moja

ya China ilibadilishwa kwa watani wa TZS 6.96 mwaka 2022/23 ikilinganishwa na wastani wa TZS 6.45 katika kipindi kama hicho cha mwaka 2021/22. Kwa ujumla Sarafu ya Tanzania haikuathirika sana na mabadiliko ya thamani ya fedha ukilinganisha na sarafu nyengine ulimwenguni.

## 2. UTEKELEZAJI MPANGO WA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI – JUNI 2022/2023

Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2022/2023 ni mwanzo wa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) (2021-2026) ambao unalenga kutekeleza Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050. Mpango huo una jumla ya Programu 29 (programu 4 mpya) na Miradi 43 (miradi 13 mipya) ambayo imepangwa kutekelezwa na kupangiwa jumla ya TZS 1.35 trilioni. Kati ya fedha hizo, Serikali imepanga kutumia TZS 682.5 bilioni sawa na asilimia 50.5 ya Bajeti ya Maendeleo kutoka fedha za vyanzo vya ndani na TZS 669.7 bilioni sawa na asilimia 49.5 zilipangwa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ikiwa TZS 62.8 bilioni ni ruzuku na TZS 606.9 bilioni ni mikopo.

Jumla ya TZS 628.4 bilioni sawa na asilimia 46.5 ya bajeti ya Mpango wa Maendeleo zilipangwa kugharamia Programu na Miradi ya Kimkakati. Kati ya fedha hizo, TZS 279.3 bilioni sawa na asilimia 44.4 kutoka Serikalini na TZS 349.1 bilioni sawa na asilimia 55.6 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Utelezaji hali hadi kufikia Juni mwaka wa fedha 2022/2023, jumla ya TZS 460.7 bilioni sawa na asilimia 34.1 ya lengo la TZS 1,352.2 bilioni zilitumika katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo. Kati ya fedha hizo, TZS 308.9 bilioni sawa na asilimia 45.3 ya lengo la TZS 682.5 bilioni zilitoka Serikalini na TZS 151.8 bilioni sawa na asilimia 22.7 ya lengo la 669.7 bilioni zilitoka kwa Washirika wa Maendeleo. Mchanganuo wa

upatikanaji fedha kwa programu na miradi kwa kipindi hicho unaonekana katika ***Kiambatisho namba...***

## 3. UTEKELEZAJI WA BAJETI JULAI - JUNI 2022/2023

### *3.1 MAPATO*

Serikali imechukua jitahada mbali mbali katika sera zake na kusimamia vipengele tofauti kwa ajili ya uongezaji wa mapato ya ndani kwa mantiki ya kupunguza utegemezi wa misaada kutoka nje. Vipengele hivi vinajumuisha uongezaji wa ukusanyaji wa mapato kwa kuimarisha vyanzo vilowepo na kutambua vyanzo vyengine vya ukusaji wa mapato

Kwa mwaka wa fedha 2022/23, Serikali ilipanga kukusanya jumla ya TZS 2,572.7 bilioni kati ya fedha hizo TZS 1,234.1 bilioni kutokana na mapato ya ndani na TZS 1,338.6 bilioni mapato mengineyo.

#### *3.1.1 Mapato ya Ndani*

Mapato ya ndani yaliyopangwa kwa kipindi cha Julai-Juni mwaka wa fedha 2022/23, yatokanayo na kodi ni TZS 1,054.7 bilioni na mapato yasiyokuwa ya kodi ni TZS 179.5 bilioni. Kati ya mapato hayo ya kodi Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) ilipangiwa kukusanya jumla ya TSZ 579.5 bilioni na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) TZS 454.1 bilioni

#### *3.1.2 Mapato Mengineyo*

Kwa upande wa mapato mengineyo kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Serikali ilikadiria kukusanya Jumla ya TZS 1,054.7 bilioni yakihusisha mkopo wa ndani wa TZS 115.0 bilioni, mkopo kwa ajili ya miradi ya maendeleo TZS 400.0 bilioni, mapato kutoka nje TZS 677.7 bilioni, marejesho ya mkopo kutoka Exim Bank ya

China TZS 130.4 bilioni, Msaada wa Kibajeti wa TZS 10.0 bilioni na TZS 0.2 bilioni ni Mfuko wa Pamoja wa Fedha.

#### *3.1.3 Utekelezaji Halisi*

Kwa kipindi kilichoishia Juni wa mwaka wa fedha 2022/2023, mapato ya Serikali yalifikia TZS 1,590.3 bilioni sawa na asilimia 61.8 ya makisio ya ukusanyaji wa TZS 2,572.7 bilioni. Makusanyo haya yanajumuisha mapato ya ndani ya TZS 1,193.1 bilioni na mapato mengineyo ya TZS 397.3 bilioni.

Katika kipindi hicho, ukusanyaji halisi wa mapato ya ndani umefikia TZS 1,193.1bilioni sawa na asilimia 96.7 ya makadirio ya ukusanyaji wa TSZ 1,234.1 bilioni, ukusanyaji huu umeongezeka kwa asilimia 34.2 ukilinganisha na kipindi kama hiki kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo jumla ya TZS 889.1 billioni zilikusanywa.

Makusanyo yatokanayo na kodi yamefikia TZS 1,038.3 bilioni sawa na asilimia 98.5 ya makadirio ya ukusanyaji wa TZS 1,054.6 bilioni na kumejitokeza ongezeko la asilimia 38.3 ukilinganisha na kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo mapato ya kodi yalifikia TZS 751.0 bilioni. Aidha mapato yasiyokuwa ya kodi yameripotiwa TZS 154.8 bilioni sawa na asilimia 86.2 ya makadirio ya TZS 179.5 bilioni, mapato yasiyo ya kodi nayo yameongezeka kwa asilimia 12.1 ukilinganisha kipindi kama hiki kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo jumla ya TZS 138.1 billioni zilikusanywa.

Kwa kipindi cha Julai-Juni mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya fedha zilizopatikana kutokana na mikopo na ruzuku ni TZS 172.4 bilioni sawa na asilimia 25.4 ya matarajio ya TZS 677.7 bilioni, ikilinganishwa na kipindi kama hicho

mwaka wa fedha 2021/2022 ambapo jumla ya TZS 173.3 bilioni zilipatikana kunajitokeza upungufu wa TZS 0.84 bilioni.

Vile vile kwa kipindi hicho cha mwaka wa fedha 2022/2023 jumla ya fedha zilizopatikana kutokana na Msaada wa Kibajeti ni TZS 67.4 bilioni sawa na asilimia 674.3 ya matarajio ya TZS 10.0 bilioni, Marejesho ya Mkopo wa Exim Benki ya China yalifikia TZS 130.4 bilioni sawa na asilmia 96.1 ya matarajio ya ya TZS 135.7 bilioni na TZS 27.0 blioni zilipatikana kutokana na Serikali kukopa kwa ajili ya Miradi Maendeleo ambapo sawa na asilimia 6.8 ya matarajio ya kukopa TZS 400.0 bilioni. **Jadweli na 1 linaonyesha mchanganuo wa mapato kwa mwaka wa fedha 2022/2023**

**Jadweli namba 1**

| MAPATO | | | | |
|---|---|---|---|---|
| JULAI -JUNI | | | | bilioni' |
| | 2021/2022 | 2022/2023 | | |
| **Maelezo** | **Halisi** | **Bajeti** | **Halisi** | **Aslimia** |
| **Mapato ya Ndani** | **889.1** | **1,234.1** | **1,193.1** | **96.7** |
| ZRB | 374.3 | 579.5 | 565.9 | 97.6 |
| Mapato yasiyokuwa ya Kodi | 138.1 | 179.5 | 154.8 | 86.2 |
| TRA | 355.7 | 454.1 | 451.4 | 99.4 |
| Mapato - Wafanyakazi wa SMT | 21.0 | 21.0 | 21.0 | 100.0 |
| **Mapato Mengineyo** | **545.8** | **1,338.6** | **397.3** | **29.7** |
| Mkopo wa Ndani | 140.0 | 115.0 | - | - |
| Mapato kutoka Nje | 173.3 | 677.7 | 172.4 | 25.4 |
| Msaada wa Kibajeti (GBS) | 2.3 | 10.0 | 67.4 | 674.3 |
| Marejesho ya Mkopo Exim Bank China | | 135.7 | 130.4 | 96.1 |
| Mkopo kwa Miradi ya Maendeleo | | 400.0 | 27.0 | 6.8 |
| Mfuko wa Pamoja wa Fedha | | 0.2 | - | - |
| Mkopo -IMF | 230.2 | - | - | - |
| **Jumla** | **1,434.9** | **2,572.7** | **1,590.3** | **61.8** |
| ***Chanzo: Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali*** | | | | |

### *3.2 MATUMIZI*

Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Serikali ilikadiria kutumia jumla ya TZS 2,572.7 bilioni, ikihusisha matumizi ya kazi za kawaida ya TZS 1,220.5 bilioni na kazi za maendeleo TZS 1,352.2 bilioni.

Katika kipindi hicho jumla ya matumizi ya kawaida, mishahara ilikadiriwa TZS 628.7 bilioni, matumizi mengeniyo TZS 381.5 bilioni na matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali TZS 210.3 bilioni.

Kwa upande wa makadirio ya shughuli za maendeleo, Serikali ilikadiria kutumia TZS 682.5 bilioni zitokanazo na makusanyo ya ndani na TZS 669.7 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ikuhusisha Ruzuku na Mikopo.

Kwa kipindi cha Julai-Juni mwaka wa fedha 2022/2023, matumizi halisi yalifikia jumla ya TZS 1,453.7 bilioni, yakijumuisha matumizi yatokanayo na Fedha za ndani ya jumla ya TZS 1,301.9 bilioni na TZS 151.8 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Kati ya matumizi hayo, TZS 993.0 bilioni zimetumika kwa matumizi ya kawaida sawa na asilimia 81.4 ya makadirio ya TZS 1,220.5 bilioni na matumizi kwa miradi ya maendeleo yalifikia TZS 460.7 bilioni sawa na asilimia 34.1 ya makadirio ya TZS 1,352.2 bilioni.

Jumla ya matumizi halisi ya kawaida ya TZS 993.0 bilioni, mishahara imefikia TZS 626.9 bilioni sawa na asilimia 98.8 ya makadirio ya TZS 628.7 billion, matumizi mengineyo ya ofisi yamefikia TZS 194.4 bilioni sawa na asilimia 60.0 ya makadirio ya

TZS 381.5 bilioni na Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali yamefikia TZS 171.7 bilioni sawa na asilimia 81.7 ya makadirio ya TZS 210.3 bilioni.

Kwa upande wa matumizi halisi ya miradi ya maendeleo ya TZS 460.7 bilioni, jumla ya TZS 308.9 bilioni zimetokana na fedha za mapato ya ndani ambapo ni sawa asilimia 45.3 ya makadirio ya TZS 682.5 bilioni na jumla ya TZS bilioni 151.8 bilioni zimetokana na Washirika wa Maendeleo ikihusisha ruzuku na mikopo sawa na asilimia 22.7 ya makadirio ya TZS 669.7 bilioni. **Jadweli na 2 na 3 linaonyesha mchanganuo wa matumizi kwa mwaka wa fedha 2022/2023**

**Jadweli namba 2**

| MATUMIZI | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **JULAI -JUNI** | | | | **bilioni'** |
| | **2021/2022** | **2022/2023** | | |
| **Maelezo** | **Halisi** | **Bajeti** | **Halisi** | **Aslimia** |
| **Matumizi ya Kawaida** | **740.9** | **1,220.5** | **993.0** | **81.4** |
| Mshahara Mawizara | 343.2 | 558.0 | 528.0 | 94.6 |
| Mfuko Mkuu wa Serikali | 167.7 | 210.3 | 171.7 | 81.7 |
| Mishahara Ruzuku | 71.1 | 70.7 | 98.8 | 139.7 |
| Matumizi Mengineyo Ruzuku | 46.8 | 116.2 | 63.9 | 55.0 |
| Matumizi Mengineyo Wizara | 100.4 | 265.4 | 130.5 | 49.2 |
| Matumizi ya Uviko 19 | 11.5 | - | - | |
| Matumizi ya Kawaida-Wahisani | 0.2 | - | | |
| **Matumizi ya Maendeleo** | **466.2** | **1,352.2** | **460.7** | **34.1** |
| Fedha za Serikali | 139.7 | 682.5 | 308.9 | 45.3 |
| Fedha kutoka Washirika wa Maendeleo | 173.3 | 669.7 | 151.8 | 22.7 |
| Mkopo kutoka IMF | 153.3 | | | |
| **Jumla** | **1,207.1** | **2,572.7** | **1,453.7** | **56.5** |
| ***Chanzo: Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali*** | | | | |

**Jadweli namba 3**

| Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **JULAI -JUNI** | | | | **bilioni'** |
| | **2021/2022** | **2022/2023** | | |
| **Maelezo** | **Halisi** | **Bajeti** | **Halisi** | **Aslimia** |
| Malipo ya Mishahara ya Viongozi Wakuu | 1.22 | 2.50 | 2.40 | 96.00 |
| Malipo ya mafao ya Kiinua mgongo | 32.59 | 25.00 | 20.20 | 80.80 |
| Malipo ya Pencheni kwa wastaafu wa SMZ | 31.20 | 35.00 | 32.60 | 93.14 |
| Malipo ya Mikopo ya ndani | 39.55 | 27.90 | 23.30 | 83.51 |
| Matumizi Maalum ya Serikali | 63.66 | 94.90 | 81.20 | 85.56 |
| Marejesho ya Mkopo wa ZSSF | - | 26.30 | 12.00 | 45.63 |
| **Jumla** | **168.22** | **211.60** | **171.70** | **81.14** |
| *Chanzo: Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali* | | | | |

### *3.3 DENI LA TAIFA*

Deni la Taifa hadi kufikia Juni, 2023 limefikia TZS 354.8 bilioni, ambapo kati ya deni hilo, deni la ndani ni TZS 341.4 bilioni sawa na 96% na deni la nje linalodhaminiwa na Serikali ya mapinduzi ya Zanzibar ni TZS. 13.3 bilioni sawa na 4% ya deni lote.

Deni la ndani linatokana na mikopo ya Hati fungani za muda mrefu (Treasury Bond), Hati fungani Maalum za Benki Kuu (BOT Special Bond) pamoja na mkopo wa Mfuko wa Hifadhi wa Jamii Zanzibar (ZSSF). Hati fungani Maalum zilizochukuliwa kutoka Benki Kuu ya Tanzania zimefikia TZS 120.0 bilioni, Hatifungani kutoka sokoni TZS 159.5 na mikopo kutoka Mfuko wa Hifadhi wa Jamii (ZSSF) umefikia TZS 61.9 bilioni.

Hadi kufikia Juni 2023 Deni la Nje linalodhaminiwa na SMT kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Zanzibar limefikia TZS 2,396.4 bilioni.

### *3.4 HITIMISHO*

Naomba Wajumbe wa Kamati yako ya Bajeti waipokee, waijadili na hatimae waishauri Serikali katika maeneo ambayo yatahitaji kuimarishwa zaidi ili kufikia malengo ya Bajeti ya Serikali kama yalivyoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi.

**SADA S. MKUYA**

**WAZIRI WA NCHI OR- FEDHA NA MIPANGO,**
**ZANZIBAR.**

**Ogasti, 2023**